

NJIA YA MSALABA

Frt. Ignat Muondezi

Tar. 12, March, 2022

Kibosho Senior Seminary

Grave

$\text{♩} = 68$

Tu fu a te nji a ya msa la ba Tu i fwa te mpa ka Kal
 va ri o Tu si ma me po bi la ha ya. Msa la - ba
 hu o
 msa la ba hu o msa la ba hu po nya ro ho.

- | | |
|--|---|
| <ol style="list-style-type: none"> Umekosa nini we Yesu
Kushtakiwa bure kwa Pilato
Wenye kustahili hukumu
Siwewe (Bwana), si wewe (Bwana) si wewe
Bwa-na ni sisi.x2 Ole wa msalaba huo mzito
Apagazwa mwana mpenzi wa Mungu
Mwili waenea mateso
Alipa (dhambi), alipa (dhambi), alipa ma-dhambi yetu.x2 Ona Muumba mbingu na nchi
Yupo chini mzigo wamwelemea
Na mtu kiumbe chake kwa ukali | <ol style="list-style-type: none"> Ampiga (Bwana), ampiga (Bwana) ampiga
bi-la huruma. Huko njiani we Maria
Waonaje hali ya Mwanaao
Ni damu tupu na vidonda
Machozi (Bwana), machozi (Bwana),
machozi ya-mfumba macho.x2 Kwa Simoni heri ya kweli
Mimi pia Yesu nisaidie
Kuchukua mzigo wa ukombozi
Kuteswa (nawe), kuteswa (nawe) kuteswa
pa-moja nawe.x2 |
|--|---|

- | | |
|--|--|
| <p>6. Uso wa Yesu malaika
Betlehemu walikuabudu
Bahati yake Veronika
<u>Kupangusa</u> (mfalme), <u>kupangusa</u> (mfalme),
kupangusa mfa-lme wa Mbingu.x2</p> <p>7. Wakimvuta huku na huku
Wauaji wanamchokesha bure
Chini wamtupa bado kwa nguvu
Aibu (yao), aibu (yao), aibu ya-o milele.x2</p> <p>8. Wanawake wa Israeli
Musilie kwa sababu hiyo
Muwalilie hao kwa dhambi
Upanga (kwao), upanga (kwao), upanga ni-
juu yao.x2</p> <p>9. Mwokozi sasa ni ya tatu
Waanguka chini ya msalaba
Katika dhambi za uregevu
Nijue (mimi), nijue (mimi), nijue ku-tubu
hima.x2</p> <p>10. Muje malaika wa Mbingu
Funikeni mwiliwe kwqa huruma
Vidonda vyake na utupu
Askari (nao), askari (nao), askari wa-
memvua.x2</p> <p>11. Hapo mkristu ushike moyo
Bwana wako alazwa msalabani
Mara miguu na mikono
Yafungwa (kweli), yafungwa (kweli)
yafungwa kwa-misumari.x2</p> <p>12. Yesu mpenzi nakuabudu msalabani
Msalabani unapohangaika
Nchi yatetemeka kwa hofu
Na jua (nalo), na jua (nalo), na jua li-
nafifia.x2</p> <p>13. Mama Maria Mtakatifu
Upokee maiti ya Mwanao
Tumwemwua kwa dhambi zetu
Twatubu (kwake), twatubu (kwake),
twatubu kwa-ke na kwako.x2</p> <p>14. Pamoja nawe kaburini
Zika dhambi na ubaya wa moyo
Yesu tuwe wakristu kweli
Twakupa (sasa), twakupa (sasa), twakupa
sa-sa mapendo.x2</p> | <p>15. Katika roho yangu Bwana
Chora mateso niliyokutesa
Nisiyasahau madeni
Na kazi (Bwana), na kazi (Bwana), na kazi
ya-kuokoa.x2</p> |
|--|--|